



National Council of NGOs
S.L.P 32088, DAR ES SALAAM - TANZANIA
SIMU: +255 754 310094, +255 754 392936



TAMKO LA ASASI ZA KIRAIA KUHUSU MUSWADA WA MABADILIKO YA SHERIA MBALIMBALI ZINAZOONGOZA ASASI ZA KIRAIA NCHINI

1.0 Utangulizi

Ndugu Waandishi wa Habari

Sisi Asasi za Kiraia na Wadau zaidi ya 325 kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu, tumekutana leo hapa jijini Dar es Salaam, katika mkutano wa dharura ulioandaliwa kwa pamoja kati ya Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) na Chama cha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania (TANGO).

Lengo kuu la mkutano huu ni kujadili kwa pamoja Muswada wa mabadiliko ya Sheria mbalimbali zinazoongoza Asasi za Kiraia na baadae kufikisha kilio chetu kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ili waweze kurekebisha vifungu ambavyo, kama Muswada huu utapita kutakua na mazingira magumu ya utendaji kazi wa Asasi za Kiraia ikiwemo kufutwa kwa baadhi ya Asasi nchini.

2.0 Kuhusu Muswada

Mnamo tarehe 19//June/2019, kwa hati ya dharura Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria mbalimbali katika nchi yetu. Muswada huu uliowasilishwa kwa dharura umezua sintofahamu na taharuki kwa Asasi za Kirai (AZAKI) za ndani na za nje ya nchi. Swala hili limeacha maswali mengi na mshangao mkubwa kwa Taifa hasa lengo la kutokushirikisha AZAKi ambao ni walengwa wakuu kwenye muswada huo. Miongoni mwa sheria hizo ni Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002, Sheria ya Jumuiya za Kijamii, Sheria ya Mabaraza ya Wadhamini na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Sheria hizi nne ni miongoni mwa sheria kuu zinazoongoza Asasi za Kiraia Nchini.

Tarehe 21 na 22 mwezi Juni 2019 baadhi ya AZAKi ziliweza kuwasilisha maoni yetu mbele ya kamati za Bunge mjini Dodoma. Leo pia tumekutana hapa kwa dharura ili kujadili mapendekezo yetu na kuuhabarisha umma kuhusu Muswada huu. Umma unapaswa kujua

kuwa muswada huu ukipita hautaathiri AZAKI peke yake bali kila mtu ataathirika kwakuwa AZAKI zipo kwa ajili ya kutoa huduma mbali mbali za kijamii, kuleta maendeleo na ajira katika nyanja mbali mbali.

Sekta ya AZAKI nchini inamchango mkubwa sana kwa Taifa katika nyanja tofauti. Mfano Sekta hii hutoa ajira kwa mamilion ya wataanzania Bara na Visiwani. Sekta hii pia ina mchango mkubwa katika sekta zingine kama ya Afya, Elimu na Kilimo. Mashirika mengi pia yanasadia Serikali kulinda na kutetea haki mbalimbali za raia pamoja na mengine mengi kama kulipa kodi na kuleta fedha za kigeni nchini. Hivyo basi kuendelea kutunga sheria kandamizi kwa sekta hii ni sawa na kupanga kulimaliza Taifa kwa ujumla kwa kuwa waathira ni wengi na Taifa kwa ujumla.

Ndugu Waandishi wa Habari

Kutokana na uchambuzi wa awali uliofanywa na Asasi za Kiraia zaidi ya 300 kuhusu Muswada huu, ikiwa Muswada huu utapita kama ulivyo sasa, utaleta changamoto nyingi katika utekelezaji wake na uendeshaji wa AZAKi nchini. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuminywa kwa uhuru wa AZAKI nchini kinyume na katiba pamoja na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia, Msajili wa NGOs amepewa mamlaka makubwa bila kudhibitiwa ya namna ya kusimamia AZAKi ikiwa ni pamoja na kusimamisha usajili wa AZAKI pasipo kufuata utaratibu wa kisheria.

3.0 Changamoto za Muswada

Baada ya kuupitia Muswada huu sisi Asasi za Kiraia tumeona changamoto na madhara yafuatayo yatatokea endapo Muswada huu utapita:

1. Muswada huu utazitaka AZAKI zote zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni ambayo hayakuomba Hati ya kukubaliwa kufanya kazi kama Mashirika yasiyokua ya Kiserikali chini ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002 yatatatakiwa kufanya kazi kama Makampuni ya Kibiashara kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni na iwapo yatashindwa kufanya hivyo ndani ya muda wa miezi miwili yatafutwa usajili bila ya kupewa taarifa.

2. Muswada unaopendekezwa unafuta tafsiri iliyopo ya neno Shirika lisilokuwa la Kiserikali na kuleta tafsiri mpya ambayo haitambui nyanja ya ulinzi, utetezi na uendelezaji wa haki za binadamu nchini Tanzania, na ikumbukwe kuwa mpaka sasa hakuna Sheria nchini inayowatambua watetezi wa haki za binadamu. Sheria pia haijatambua mashirika yanayolinda haki za watu wenye ulemavu, makundi maalum na wengine wengi. Sheria hii imeshindwa pia kuelezea kuwa sekta ya AZAKI ni ya kujitolea kuhudumia jamii (Charities). Makundi ya AZAKI na mashirika ya kimataifa pia hayajatambuliwa katika tafsiri hii. Pia tafsiri hii mpya haijumuishi makampuni yasiyokuwa na hisa, ambayo hayatengenezi faida (Company Ltd by Guarantee not having a share capital), makundi madogo madogo ya uwezeshaji (VIKOBWA kwa ujumla), mashirika ya dini na kadhalika. Katika Sauti hiyo hiyo, tafsiri ya neno kampuni imeminywa kuhakikisha kuwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali hayawezi tena kuwa makampuni yasiyokuwa na hisa, ambayo hayatengenezi faida. Hivyo, makampuni ni lazima yafanye biashara au uwekezaji tu ili yaweze kusajiliwa.
3. Muswada huo unaongeza kifungu cha 8A ambacho kinafuta usajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yamesajiliwa chini ya sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs Act, 2002), ambayo hayajajumuishwa kwenye tafsiri hii mpya, ndani ya miezi miwili baada ya Muswada huu kupitishwa kuwa Sheria. Hatua hii inakiuka uhuru wa kujumuika ambao unalindwa na Katiba pamoja na mikataba ya kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia. Ni muhimu njia mbadala zitolewe kwa mashirika haya halali kuhamia katika upande unaofaa na sio kufutiwa usajili moja kwa moja.
4. Muswada huo unarekebisha Kifungu cha 4(1) kwa kuongeza vipengele ambavyo vinaruhusu kusimamishwa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali bila kupewa haki ya asili na ya kikatiba ya kusikilizwa wakati yakingojea uamuzi wa Bodi, kitu ambacho ni kinyume na Kanuni za Haki; dhana ya kutokuwa na hatia ambayo ni msingi wa haki uliopo kikatiba. Shirika linatakiwa kusimaishwa baada ya kuthibitika kuwa na hatia mbele ya Bodi.
5. Kifungu cha 4(1) kimerekebishwa pia kuongeza kipengele kinachompa Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali mamlaka makubwa ikiwemo kufuatilia na kutathmini mashirika yasiyo ya kiserikali kila baada ya robo mwaka. Mamlaka hayo

hayajadhibitiwa na Sheria ipasavyo. Mamlaka kama haya yanaweza kutumika kiholela, vibaya na kwa kuonea. Hatuna shida na kutembelewa na Msajili kw hata sasa anayofursa ya kutembelea ila swala la kuweka kuwa ni kila miezi 3 huenda ikalazimisha AZAKI kudaiwa kutuma taarifa kila robo mwaka kwa ni ngumu kutembelea wote.

6. Kifungu cha 4 kimefanyiwa marekebisho na kumpa uwezo Msajili kuchunguza mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kushirikiana na vyombo vya dola. Mamlaka kama haya yanahusishwa na udhibiti ambao unaingilia haki ya faragha na uhuru wa Shirika. Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali hapaswi kupewa mamlaka chini ya Sheria nyingine yoyote kufanya uchunguzi wa uhalifu. Wigo wa sheria yoyote nyingine iliyoandikwa haujulikani na hii inaweza kuvutia matumizi mabaya ya mamlaka haya na kupelekea kukamatwa kiholela na kuingiliwa kwa wahusika wa AZAKI. Msajili abaki kuwa mlezi na mshauri wa AZAKI.
7. Kifungu cha 17 kinaondoa usajili wa kudumu wa AZAKI. Kifungu hicho kinayataka mashirika yasiyo ya kiserikali kujisajili upya/ kupata hati za usajili mpya kila baada ya miaka 10. Huu ni mzigo kwa mashirika yasiyo ya kiserikali kiuchumi na kiutawala, lakini pia ni mzigo kwa ofisi ya Msajili wa NGOs. Utaratibu huu unaondoa uhuru wa mashirika yasiyo ya kiserikali na kujenga woga, hofu na udhibiti binafsi. Utaratibu huu utawafanya wafadhili waogope kuingia mikataba mirefu na AZAKI kwani uhakika wa kupata cheti utakuwa ni mdogo baada ya miaka 10. Tunashauri AZAKI zisajiliwe na kupewa usajili wa kudumu.
8. Kifungu cha 38 cha Sheria ya Jumuiya za Kijamii (the Societies Act) kinampa Waziri mwenye dhamana mamlaka ya kutamka kuwa Asasi/ Jumuiya Fulani ya kijamii kuwa ni hatari kwa utawala bora nchini na akitamka hivyo, Asasi/Jumuiya hiyo inakuwa sio halali kuendelea kufanya kazi. Kifungu hiki kinampa mwanya Waziri kutumia mamlaka yake vibaya na kufanya Asasi/Jumuiya nchini kuishi kwa hofu ya kutamkwa kuwa sio halali. Makosa ambayo ni hatari kwa utawala bora ni ngumu kuyatambua.
9. Asasi za Kiraia zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni ambazo hazina hisa, na hazitengenezi faida (Company Ltd by Guarantee not having a share capital) na hazikuomba cheti cha ukubalifu kwa msajili wa NGOs chini ya kifungu cha 11 cha Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali, zinatakiwa kukubaliana na sheria ya

makampuni na kuwa mashirika ya kibiashara, lasivyo zitafutiwa usajili baada ya Muswada huu kupita kuwa Sheria.

10. Kwa mujibu wa mabadiliko haya sheria ya Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali hayatakua tena na nafasi katika nafasi katika kupendekeza wawakilishi wao katika Baraza la Mashirika yasio kuwa ya Kiserikali, kinyume na taratibu za kidemokrasia. Mswada huu unakwenda pia kupunga kazi za Baraza kama chombo cha kujitathmini cha AZAKI.

4.0 Wito Wetu

Kutokana na changamoto hizo pamoja na madhara ya Muswada huu, sisi Asasi za Kiraia tunapendekeza yafuatayo:

- i. Tunawaomba Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuusoma kwa makini na kuuelewa Muswada huu na hatimaye watakapokua ndani ya Bunge waweze kutoa Mapendekezo ya kurekebisha na kuboresha vipengele vyote vinavyoathiri AZAKI nchini.
- ii. AZAKI nchini ziungane na ziendee kufanya ushawishi kwa wabunge na serikali madhara ya kupitisha Muswada kuwa sheria.
- iii. Sisi Asasi za Kiraia tunaomba muswada huu uondolewe kwenye hati ya dharura na tushirikishwe katika hatua zote ikiwa ni pamoja na kukusanya maoni yetu na kuzingatiwa. Sisi ndio wadau na waathirika namba moja wa muswada huu.
CSOs in Tanzania requests that the proposed Bill be removed from
- iv. Tunawaomba wadau wote wa nje na ndani kushikamana kwa pamoja na kupaza sauti zetu ili kuhakikisha Muswada huu haupiti na kuwa sheria.
- v. Tunaomba wadau wote hapa nchini pamoja na raia kwa ujumla watusaidie kushawishi Muswada huu urudi kwa ajili ya majadiliano zaidi na AZAKI.
- vi. Endapo Muswada huu utapitishwa kama ulivyo sasa na kuwa sharia sisi Asasi za Kiraia tupo tayari kwenda mahakamani kuupinga kwakuwa athari zake nikubwa kuliko manufaa.

- vii. Tunaomba Kamati ya Bunge muyapokee mapendekezo yetu ambayo siku ya leo tumeyakamilisha ili kuongezea yale ambayo tayari yalishafika kwenu kutoka kwetu siku ya awali.

IMETOLEWA LEO TAREHE 24 JUNI 2019

Na Wadau na AZAKI 325 kama ifuatavyo;

1. ABDALA ABEID-ZAFAYCO
2. ACT – MARA DIOCESE – MUGUMU SAFE HOUSE
3. ACTION AID
4. ACTION FOR DEMOCRACY AND LOCAL GOVERNANCE
5. AGAPE AIDS CONTROL PROGRAM
6. AGNES HAULE-AICIL
7. AHADI FORUM TANZANIA (AFTA)
8. ALEX I. LUOGA-YAAPA-KIGOMA
9. ANTONY MAYUNGA
10. ARUSHA NON GOVERNMENTAL ORGANISATION NETWORK(ANGONET)
11. ARUWE
12. ASSOCIATION FOR NON GOVERNMENTAL ORGANISATION ZANZIBAR
13. ASSOCIATION OF RARE BLOOD DONOR
14. ASTRONOUT BALIGE-WISE
15. ATAHRA
16. AUGUST MGENDI
17. AVIWATA
18. AWWORIT
19. BALNSI CHINA
20. BALTAZER KOMBA-FAWOPA
21. BB DOMINIC
22. BENSON ASWILE
23. BETTER LIFE
24. BHR
25. BIHARAMULO COMMUNITY FM RADIO
26. BIHARAMULO NGOS NETWORK FORUM
27. BIHARAMULO ORIGINATING SOCIAL ECONOMIC DEVELOPMENT ASSOCIATION (BOSEDA)
28. BIHARAMULO SOCIAL ECONOMIC DEVELOPMENT ASSOCIATION (BISEDEA)
29. BINGOS FORUM
30. CENTER FOR YOUTH DIALOGUE (CYD)
31. CESOPE
32. CHIBURA MAKORONGO
33. CHIFU KIMWERI FOOTBALL CLUB

34. CHILD WATCH
35. CHILDREN DIGNITY FORUM
36. CHRISTIAN EDUCATION AND DEVELOPMENT ORGANIZATION (CEDO)
37. CHRISTINA KAMILI RUHINDA-TANLAP
38. CHRISTINE AVIAH
39. CIVIC AND LEGAL AID ORGANISATION
40. CLAUDINA A HAULI-AHADI FORUM
41. COMMUNITY DEVELOPMENT INITIATIVES SUPPORT ORGANIZATION (COSIDO)
42. COMMUNITY FOCUS TANZANIA
43. COMMUNITY FOR EDUCATORS AND LEGAL ASSISTANCE
44. COMMUNITY SUPPORT INITIATIVES
45. CORDS
46. COSITA
47. CRISIS RESOLVING CENTER
48. C-SEMA
49. CWCA
50. DAVID CHANYEGHEA-NEW AGE FOUNDATION
51. DAWNING HOPE
52. DEO NSOKOLO-UTPC
53. DEUS M KIBAMBA-JUKATA
54. DIGNITY KWANZA COMMUNITY SOLUTIONS
55. DOOR OF HOPE TO WOMEN AND YOUTH TANZANIA
56. DUNGONET (NGOS NETWORK FOR DODOMA)
57. EDWIN SOKO-OJADACT
58. ELIZABETH NKAINA-IGT
59. EMMANUEL EUSTACE
60. EMPOWER SOCIETY , SAVE LIVES; JUMUIYA YA KUTETEA WANAWAKE NA WATOTO SHRHIYA YA OLE
61. EMPOWERMENT SOCIETY TRANSFORM LIVES.
62. EQUALITY FOR GROWTH
63. ERICK LUWONGO-HAKI MADINI
64. ESTL-TANZANIA
65. EVELYNE LYIMO-SMCCT
66. EVENA MASSAE-COSUPED
67. FAWETZ
68. FESTO MRINA-TAWEA
69. FICOFawe WPMEN EMPOWERMENT
70. FIDELIS YUNDE-YOUTH MOVEMENT FOR CHANGE –SINGIDA
71. FLORA MASOY-MOROGORO PARALEGAL CENTRE
72. FORTUNATA MANYERESA
73. FRANCIS GODWIN
74. FRANK MGUNDA
75. FREDRICK FUNGO-TAWEDO
76. FREE MIND FOUNDATION
77. GABRIEL JOHN-PPJ
78. GELINE ALFRED FUKO-TIFLD
79. GERALD NGO'NGA'-RAFIKI-SDO
80. GIDION KAINO MANDESI-DOLASED

81. GIRLS EDUCATION SUPPORT INITIATIVES
82. GIYEDO
83. GODPHREY PHILIMON
84. GOSPEL COMMUNICATION NETWORK OF TANZANIA
85. GOWIN MSALICHUNA
86. GROWTH DIMENSIONS AFRICA
87. HAKI CATALYST
88. HAKI ELIMU
89. HAMZA R. SUNGHE
90. HAPPY CHILDREN TANZANIA ORGANISATION
91. HILDA S.DADU-PHLI
92. HIMS ARUSHA
93. HUHESO FOUNDATION
94. HUMAN RIGHTS NATIONAL ASSOCIATION OF EDUCATION FOR
WORLD PEACE
95. HUMANITY AID FOR DEVELOPMENT ORGANISATION
96. HURUMA ORGANIZATION
97. INITIATIVE FOR GOOD GOVERNANCE AND TRANSPARENCE IN
TANZANIA (IGT)
98. ISRAEL ILUNDE
99. JACKSON MURO-CEDESOTA
100. JAMII MEDIA
101. JAMILA JUMA
102. JANET MAWINZA-WAJIKI
103. JAPHET KALEGEYA-CEDO
104. JARUO KAREBE-PLAJC
105. JEREMIA WANDILI-WIDE
106. JIMMY LUHENDE-ADLG
107. JOAN CHAMUNGU
108. JOHN NGINGA-TUPACE
109. JOHN SEKA-SEKA AND ASSOCIATES ADVOCATES
110. JOSHUA LISSU NTANDU-ESTL, SINGIDA
111. JUDIH ZEBEDAYO-ATAHRA
112. JUKWAA LA KATIBA
113. JUMA KAPIPI
114. JUMA MWESIGWA
115. JUMAVIWACHA LIWALE FARMERS ASSOCIATION
116. JUMUIYA YA KUELIMISHA ATHARI ZA MADAWA YA
KULEVYA , UKIMWI NA MIMBA KATIKA UMRI MDOGO
117. JUMUIYA YA KULINDA NA KUTETEA HAKI ZA WANAWAKE
NA WATOTO MKOANI
118. JUMUIYA YA MAENDELEO YA ELIMU KWA WATOTO
PEMBA
119. JUMUIYA YA MAENDELEO YA WAVUVI KOJANI
120. JUMUIYA YA MAENDELEO ZIWANI
121. JUMUIYA YA OWEDE
122. JUMUIYA YA TUMAINI JIPYA PEMBA
123. JUMUIYA YA TUSISHINDWE DEVELOPMENT
ORGANISATION
124. JUMUIYA YA WASAIDIZI WA SHERIA PEMBA

125. JUSTA MWAITUKA
126. KAGERA HUMAN RIGHTS DEFENDERS & LEGAL AID
SUPPORT ORGANISATION
127. KARENY MASASI
128. KENNETH SIMBAYA
129. KHAMIS SULEIMAN MASOUD-JUKUNUM
130. KIGOMA PARALEGAL AID CENTRE(KIPACE)
131. KIGOMA UJJI NON GOVERNMENTAL ORGANISATION
NETWORK
132. KIGOMA WOMEN DEVELOPMENT
133. KIKUNDI CHA USHINDI
134. KIUNGONET
135. KIWOHEDE
136. KOK FOUNDATION
137. LAETITIA PETRO-SAUTI YA HAKI TANZANIA
138. LARETOK-LE-SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU
NGORONGORO (LASHEHABINGO)
139. LHRC
140. LINDI REGIONAL PRESS CLUB
141. LIWALE FARMERS ASSOCIATION
142. MACCLEAN MWAMLANGALA
143. MAGATA PRIMARY COOPERATIVE SOCIETY
144. MALIMA RUBASHA
145. MANYARA REGIONAL CIVIL SOCIETY NETWORK
146. MAPAMBANO CENTRE FOR CHILDREN
147. MARCELA FRANCIS LUNGU
148. MARCELA ILUNDE -YPC
149. MARTHA JEROME
150. MARTHINA KABISAMA
151. MBEYA HOPE FOR ORPHANS
152. MBEYA WOMEN
153. MCHOMORO AIDS COMBAT GROUP
154. MEDIA ASSOCIATION FOR INDIGENOUS AND PASTORALIST
155. MFADEO MBWENE
156. MICHAEL REUBEN NTIBIKEMA-ELIMU MWANGAZA
TANZANIA
157. MICHEWENI ISLAMIC DEVELOPMENT ENVIRONMENTAL
CONSERVATION AND AIDS CONTROL
158. MIKONO YETU CENTER FOR CREATIVITY AND
INNOVATION
159. MIRIAM CHAKWAWA-RUWODI
160. MSICHANA INITIATIVES
161. MTWARA NGOS NETWORK
162. MTWARA PARALEGAL CENTER
163. MTWARA YOUTH ANT AIDS GROUP
164. MUKEMBA GROUP MAENDELEO
165. MUSA JONAS NGANGALA-TVMC SHINYANGA
166. MUSSA JUMA-MISA TAN
167. MUSSA KOMBO MUSSA-PEMCO PEMBA
168. MWALIM SHARIF SHAPANDU-MIDECAC PEMBA

169. MWANAMKE NA UONGOZI
170. MZURI ISSA-TAMWA ZANZIBAR
171. NASSOR BILAL ALI-JUWASPE
172. NATIONAL COUNCIL OF NGOS (NACONGO)
173. NATIONAL UNION OF MINE AND ENERGY WORKERS OF TANZANIA (NUMET)
174. MAWAZO DANIEL-NYDT
175. NDAISABA GEORGE-PDF
176. NEEMA KITUNDU-FAWETZ
177. NETWO
178. NEW FAMILY ORGANISATION
179. NEW HOPE NEW WINNERS FOUNDATION (NHNWF)
180. NGUVUMALI COMMUNITY DEVELOPMENT OF ENVIRONMENT
181. NICAS NIBENGO- BASE FOR EDUCATION DISSEMINATION
182. NICODEMUS KAJUNGU
183. NOMADIC PASTORALIST DEVELOPMENT
184. NTABYMA
185. NYAKITONTO YOUTH FOR DEVELOPMENT TANZANIA
186. ODERO ODERO-CILAO
187. OPEN MIND TANZANIA
188. ORGANISATION FOR RURAL SELF-HELP INITIATIVES
189. PAMOJA DAIMA (PADA)
190. PARALEGAL PRIMARY JUSTICE
191. PATRICE GWASIMA-COSITA
192. PEACE RELIEF ORGANISATION
193. PEMBA ASSOCIATION FOR CIVIL SOCIETY ORGANISATION
194. PEMBA EAST ZONE ENVIRONMENT ASSOCIATION
195. PEMBA ISLAND AND RELIEF ORGANISATION
196. PEMCO
197. PEOPLE'S HEALTH MOVEMENT TANZANIA
198. PEOPLES DEVELOPMENT FORUM (PDF)
199. PETER BAYO-ANGONET
200. PINGOS FORUM
201. POLICY CURIOSITY SOCIETY
202. POVERTY ALLEVATION IN TANGA (POVATA)
203. PROMOTION AND WOMEN DEVELOPMENT ASSOCIATION
204. PROSPERUS HEALTH LIFE INITIATIVES
205. PWAAT
206. RACHEAL CHAGONJA-HAKI RASILIMALI
207. RAFIKI SOCIAL DEVELOPMENT ORGANIZATION
208. REHEMA JOSPHEPH-CENTA
209. RESOURCE ADVOCACY INITIATIVES
210. RIEFP
211. RODRICK MUSHI
212. ROSE SARWATT-TAWIA
213. ROWODO
214. RUNGWA ORGANISATION FOR POVERTY ALLAEVATION
215. RURAL WOMAN DEVELOPMENT INITIATIVE (RUWODI)
216. SADALINE HEALTH CARE TRUST

217. SAFE SPACE FOR CHILDREN AND YOUTH WOMEN
TANZANIA (SSCYWT)
218. SAHRINGON
219. SAID HAJI MSELLEM- ZACA
220. SAKALE DEVELOPMENT FOUNDATION
221. SALAMA AHMADA MAJALIWA-TUDOPE
222. SALMA SAID-WAHAMAZA
223. SAMMATA-ACTION FOR RURAL AID EMPOWERMENT
224. SARA KITAINDA-SHCT
225. SOPHIA DONALD-SAUTI YA WANAWAKE UKEREWE
226. SAVE THE MOTHER AND CHILDREN OF CENTRAL
TANZANIA (SMCCT)
227. SAWABI BIHARAMULO
228. SCHOLASTICA PEMBE-NHNWF
229. SERVICE HEALTH AND DEVELOPMENT FOR PEOPLE
230. SHALOM OPHARNAGE CARE CENTER
231. SHAMILA MSHANGAMA
232. SHIMAWAMI
233. SHIRIKA LA BINADAMU NANDANGALA
234. SHIVYAWATA
235. SHUKURU PAUL-HRC
236. SIKIKA
237. SOPHIA KOMBA-CAGBV
238. SORF DODOMA
239. SPORTS DEVELOPMENT AND LINDI
240. STELLA IBENGWE
241. STEPHEN WANG'ANYI
242. TAHESY
243. TALA
244. TAMHA PARALEGAL AID
245. TANDAHIMBA WOMEN ASSOCIATION
246. TANGA PARALEGAL AID
247. TANGIBLE INITIATIVES FOR LOCAL DEVELOPMENT
TANZANIA
248. TANZANIA ASSOCIATION Of NGOs (TANGO)
249. TANZANIA CENTRE FOR RESEARCH AND INFORMATION ON
PASTORALISM (TCRIP)
250. TANZANIA CITIZEN INFORMATION BERAU
251. TANZANIA HOME ECONOMIC ASSOCIATION (TAHEA)
BIHARAMULO
252. TANZANIA HUMAN RIGHTS DEFENDERS COALITION
253. TANZANIA LEGAL KNOWLEDGE AND AID CENTER
254. TANZANIA MEDIA WOMANS ASSOCIATION (TAMWA)
255. TANZANIA NATURAL RESOURCE FORUM (TNRF)
256. TANZANIA NETWORK OF LEGAL PROVIDERS (TANLAP)
257. TANZANIA NETWORK OF WOMEN LIVING WITH HIV AND
AIDS (TNW+)
258. TANZANIA PASTORALIST COMMUNITY FORUM (TPCF)
259. TANZANIA PEACE LEGAL AID JUSTICE
260. TANZANIA TOBACCO CONTROL FORUM

261. TANZANIA WIDOWS ASSOCIATION
262. TANZANIA WOMEN EMPOWERMENT IN ACTION (TAWEA)
263. TANZANIA WOMEN TEACHERS ASSOCIATION
264. TANZANIA YOUTH POTENTIAL ASSOCIATION
265. TAWASANET
266. TAWEDO
267. TECDEN
268. TEN/MET
269. TGNP MTANDAO
270. THE AFRICAN FOR CIVIL SOCIETY(TACS)
271. THE AFRICAN INSTITUTE FOR COMPARATIVE AND INTERNATIONAL LAW
272. THE FOUNDATION OF HUMAN HEALTH AND SOCIAL DEVELOPMENT (HUHESO)
273. THE FOUNDATION OF HUMAN HEALTH AND SOCIAL DEVELOPMENT INITIATIVES SUPPORT ORGANISATION
274. THE LIFE HOOD CHILDREN DEVELOPMENTS SOCIETY
275. THE ORGANISATION OF JOURNALISTS AGAINST DRUG ABUSE AND CRIMES IN TANZANIA (OJADACT)
276. THE VOICE OF MARGINALIZED COMMUNITY
277. TIBA
278. TNFR
279. TNWHIV
280. TREE OF HOPE
281. TUMAINIELI MANGI-CHILD WATCH
282. TUNDURU PARALEGAL CENTER
283. TUPACE
284. TUSHIRIK
285. TUWAANDAE WATOTO
286. TYVA
287. UMMY NDERIANANGAB-SHIVYAWATA
288. UMOJA WA VIKUNDI VYA UZALISHAJI MALI NA UELIMISHAJI RIKA MAGU (UVUUMA)
289. UMOJA WA WAWEZESHAI KIOO
290. UNDER THE SAME SUN (UTSS)
291. UTPC
292. UTTI MWANGA'MBA-CWCA
293. UVINZA NGOS NETWORK (UNON)
294. VICKY NTETEMA
295. VIJANA ASSEMBLY
296. VITAL PROJECT LIMITED
297. VOICE OF VOICELESS
298. VOLUNTEER FOR YOUTH IN HEALTH AND DEVELOPMENT
299. WAJIBU INSTITUTE OF ACCOUNTABILITY
300. WALIO KATIKA MAPAMBANO NA AIDS TANZANIA
301. WALLACE MNGOMA-HADO
302. WAMAHAZA
303. WASOMI VOICE FOUNDATION
304. WGNRR AFRICA

305. WIDOWS AND ORPHANED DEVELOPMENT ORGANIZATION
(WODEO)
306. WILDAF
307. WOFATA
308. WOMEN ACTION TOWARDS ENTER. DEVELOPMENT
309. WOMEN DIGNITY
310. WOMEN LEGAL AID CENTRE (WLAC)
311. WOMEN LIFE FOUNDATION
312. WOMEN WAKE UP
313. WOMEN'S PROMOTION CENTRE (WPC)
314. WOMENS EMPOWEREMENT IN ACTION
315. WOTE INITIATIVES
316. WOTE SAWA YOUTH DOMESTIC WORKERS
317. WOVUCTA
318. YOUTH AGAINST AIDS POVERTY
319. YUNA
320. ZAFELA
321. ZAHRA SALEHE-ICCAO
322. ZAITUNI NJIVU- ZAINA FOUNDATION
323. ZANZIBAR AIDS ASSOCIATION AND SUPPORT FOR
ORPHANS
324. ZANZIBAR CHILDREN RIGHTS FORUM
325. ZLSC